

# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI (EWURA)

### MAOMBI YA KUREKEBISHA BEI ZA MAJI YA MAMLAKA ZA MAJI SAFI NA MAJI TAKA BABATI, IGUNGA,BUKOBA,NGARA NA LIWALE

#### TAARIFA YA TAFTISHI/UCHUNGUZI (INQUIRY)

Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (*The Energy and Water Utilities Regulatory Authority (EWURA)*), imepokea maombi ya Mamlaka za Maji Safi na Maji Taka kama zilivyoanishwa hapo chini za kutaka kuongeza bei za huduma zake (*tariff adjustment*)

Na.	Mamlaka	Mwisho wa kusajili watoa maoni	Tarehe ya Taftishi	Muda	Mahali
1.	Babati (BAWASA)	21-07-07	30-07-07	03.30 Asubuhi	Ukumbi wa CCM Mkoa(Manyara)- Babati
2.	Igunga (IGUWSA)	27-07-07	02-08-07	03.30 Asubuhi	Silver B-Igunga
3.	Bukoba (BUWASA)	24-07-07	31-07-07	03.30 Asubuhi	Linas Club-Bukoba
4.	Ngara (NGUWSA)	27-07-07	02-08-07	03.30 Asubuhi	(Ukumbi wa Halmashauri ya Mji wa Ngara)
5.	Liwale (LIUWASA)	24-07-07	31-07-07	03.30 Asubuhi	(Ukumbi wa Halmashauri ya Mji wa Liwale)*

Kulingana na sheria na taratibu za EWURA (Cap 414), na kwa mujibu wa marekebisho ya sheria hii husika, EWURA itafanya mikutano ya kupata maoni kuhusiana na taftishi/chunguzi kutoka kwa wadau wa waombaji ili kujua uhalali wa maombi hayo ya kurekebisha bei za huduma zao. Nakala za maombi na nyaraka za Mamlaka hizo zilizowasilishwa EWURA zinaweza kusomwa na mtu yeyote wakati wa saa za kazi kati ya saa 3 asubuhi na saa 11 jioni katika ofisi za EWURA kwa anuani iliyotajwa hapo chini kabla ya muda ulioelekezwa hapo juu.

EWURA imeandaa mikutano itayofanyika katika maeneo husika kama ilivyoelekezwa hapo juu, ili kupata maoni ya wadau wakiwemo Baraza la wawakilishi wa watumiaji wa huduma husika (*Consumer Consultative Council -CCC*) pamoja na wadau wengine ambao ni Baraza la wawakilishi kutoka Serikalini (*Government Consultative Council-GCC*) kuhusu maombi hayoya

Mamlaka hizo. Wawakilishi wa Mamlaka wamealikwa kwenye mikutano hiyo ili washiriki kwenye taftishi/chunguzi hizo.

Wananchi wanaopenda kushiriki katika taftishi/chunguzi hizi pia wanaalikwa kuhudhuria mkutano/mikutano hiyo. Wadau wengine ambao wanapenda kutoa maoni kuhusiana na taftishi/chunguzi hizi wanakaribishwa kuleta maoni yao ki-maandishi na kuyatuma kwenye anuani iliyoonyeshwa hapa chini.

Ni wale waliojisajili tu ndio watakapata fursa ya kuwasilisha maoni yao siku hiyo ya taftishi/uchunguzi.

Wadau wengine ambao wanapenda kutoa maoni kuhusiana na taftishi/chunguzi hizi wanakaribishwa kuleta maoni yao ki-maandishi yakiambatanishwa na kiapo. Maombi hayo yatumwe kwenye anuani iliyoonyeshwa hapa katika kipindi kisichozidi wiki mbili baada ya taftish/uchunguzi kufanyika.

Ufafanuzi zaidi unaweza kupatikana kwa kuandikia EWURA. Ada ya shilingi 50,000/- inatozwa kufidia gharama za makabrasha na posta.

***Mkurugenzi Mkuu,***

***Mamlaka ya Udhhibiti wa huduma za Nishati na Maji(EWURA),***

***Ghorofa ya 6 , Harbourview Towers (zamani JM Mall Building),***

***Samora Avenue, P O Box 72175***

***DAR ES SALAAM***